**Sikiliza na Ujifunze - Mazingira na Hali ya Hewa**
**01 - 'Waste…..Takataka'**
**Text : Richard Lough**
**Redaktion und Idee : Johannes Beck**
**Translator : Mohamed Dahman**

---

Hujambo msikilizaji! Karibu katika mfululizo wa vipindi maalum vya Sikiliza na Ujifunze kuhusu mazingira. Leo tutajielimisha juu ya taathira mbaya za takataka na hususan taathira za taka za plastiki kwa mazingira yetu. Katika bara zima la Afrika suala la kukabiliana na taka ni suala ambalo serikali zimekuwa zikishindwa kulishughulikia ipasavyo. Leo katika Radionovela tutaweza kufahamu kwa kiasi gani taka za plastiki zinahatarisha maisha ya viumbe baharini na vipi uchafuzi huo unavyooua mfumo wa ekelojia baharini. Tutaangalia vipi tunaweza kupunguza kiwango cha taka tunachotoa majumbani na kujiuliza iwapo utumiaji upya wa taka unaweza kukabiliana na shinikizo linalokumba maeneo yetu ya majaa ya kutupia taka. Kadhalika tutakuwa na baadhi ya takwimu za ukweli huo kutoka kwa mwandishi wa Radio Deutsche Welle nchini Kenya, Richard Lough (anatamkwa Lock).

**Music - 0:30**

**Radionovela**

**SFX:** **Lapping waves ………sauti ya mawimbi madogo baharini**

**Gladys:** (Sigh …..akitanafusi ) …..Nakumbuka vizuri wakati ufukwe huu ulipokuwa safi sana ukiwa na mchanga mweupe na michikichi tu…

**SFX:** **Scratching up plastic bag ………sauti ya mkunjo wa mfuko wa plastki**

**Gladys:** (*Akikasirika*) Moses usitupe ovyo mfuko wako wa plastiki!

**Moses:** Kwanini nisitupe? Ni takataka ….unataka nikae nazo?

**Gladys:** Angalia jinsi pwani ilivyo siku hizi. Ni chafu haitazamiki!

**SFX:** **Picking up plastic…kuokota mifuko ya plastiki**

**Gladys:** Angalia hapa ndani ya mwani… kuna mifuko ya maduka makuu ya bidhaa, makopo ya soda, karatasi za peremende… kwa kweli inakirihisha!

**Monica:** Ndo iwe nini? Na kwa nini utake kubeba takataka zako kutwa nzima? Baba yangu siku zote huwa anarusha chupa za plastiki kutoka nje ya dirisha la gari …tena nikwambie wakati gari likiwa linakwenda.

**Gladys:** Hivyo kweli hujali juu ya mazingira yako?

**Monica:** Ahhhh… ninachojua ni kwamba sitaki kubeba takatata zangu kila ninapokweda tena kutwa nzima… na kwa nini nifanye hivyo wakati ni rahisi kuzitupilia mbali?

**Moses:** Asemayo ni kweli. Ukizingatia hakuna hata mapipa ya taka katika fukwe kwa hiyo tungelifanyaje?

**SFX:** **Music and laughter…….muziki na kicheko**

**Gladys:** Angalia hapa… hivyo unafikiri watalii huwa wanakuja kutoka mbali waliko kujianika kwenye fukwe zilizojaa taka? Hapana! Wanakuja hapa kufurahia mazingira yetu mazuri ya asili. Kwa vyovyote vile hatupaswi kuweka fukwe zetu katika hali ya usafi kwa sababu yao wao… tunalazimika kuziweka kwenye hali ya usafi kwa ajii yetu wenyewe.

**Monica:** Kweli zinaonekana chafu kutokana na kujaa taka.

**Moses:** Sasa zikionekana chafu ndio nini … hazimdhuru mtu.

**Gladys:** Aaaaaaa… hapo ndipo unapokosea Moses. Hebu njoo, nataka ukutane na kaka yangu mkubwa John.Yeye ni mvuvi katika sehemu ya chini ya ufukwe huu.

**SFX:** **Hammering nails into wood …….kugongelea misumari kwenye mbao**

**Gladys:** Habari gani John… mashua yako ina matatizo gani?

**John:** Ah, sio kitu kikubwa sana… inavuja tu kidogo. Je mnasemaje?

**Gladys:** Hebu waeleze juu ya kasa uliemuokota John …

**SFX:** **Puts down hammer …anawekwa chini nyundo yake**

**John:** Ndio siku hiyo tulikuwa tukivua kutwa nzima. Wakati tulipokuwa tukirudi ufukweni tulimuona kasa akielea juu. Nikashangaa kwa nini hakimbii wakati tulipokuwa tukimkaribia. Baadaye nikaona mfuko mweupe wa plastiki ukitoka mdomoni mwa kasa huyo.

**Moses:** Una maanisha kwamba kasa huyo alikuwa akila mfuko huo wa plastiki!

**John:** Ndio alijaribu lakini mfuko huo ulimsonga koo na kumziba pumzi.

**Monica:** (*Gasp of horror …alitweta na kuuliza kwa mshtuko*) Una maana kasa huyo alikuwa amekufa?

**John:** Unajuwa kasa huwa wanadhania mifuko hiyo ya plastiki kuwa ni kiwavi wa baharini na huwa wanapenda kula viwavi hivyo.

**Monica:** Lakini haiwezekani kuwepo kwa mifuko mingi ya plastiki kiasi hicho baharini.

**John:** Kusema kweli ipo tena mingi tu… huwa tunaiona mifuko mingi zaidi ya plastiki baharini kuliko kitu kingine chochote kile kinachotegenezwa na binaadamu. Kutokana na mfuko wa plastiki kuwa mwepesi sana inakuwa rahisi kuchukuliwa na maji baharini. Kitu kibaya zaidi ni kwamba inakuwa haiwezi kuvundishwa na bakteria.

**Gladys:** Hiyo inamaanisha nini kaka?

**John:** Ina maana kwamba viumbe hai hawawezi kuifanya plastiki ioze… kwa maneno mengine ukiwa utaitupilia mbali tu katu haitotoweka.

**Monica:** Ndio maana unaona mifuko mingi ya plastiki katika mapori na kwenye mashamba?

**John:** Ndio hasa …

**SFX:** **Traffic ………sauti ya magari**

**Moses:** Heee angalia mrundiko wa takataka ulioko pale upande wa pili wa barabara.

**Monica:** Hmm… unatoa harufu mbaya ya uvundo!

**Gladys:** (*Shriek ……..piga kelele kwa hasira* ) Doh! Kuna panya pale… nawachukia panya! Mama yangu anasema panya hubeba maradhi na daima utawakuta kwenye mirundiko ya taka.

**Monica:** Sijui kwa nini hali inafikia hivi… inaonekana hakuna mtu wa kuzoa taka kwa hiyo huwa zinaachwa ziozeane pembezoni mwa barabara. Angalia mwalimu wetu mkuu yule pale…

**Moses:** (*calls out ……anaita*) Bw.Gitanga……

**Bw.Gitanga:** Ndiyo Moses.

**Moses:** Ati ni kazi ya nani kuzoa taka barabarani?

**Bw.Gitanga:** Unajua wakati baraza la mji linapokusanya taka zetu huwa wanakwenda kuzitupa kwenye jaa la taka sio mbali kutoka hapa. Lakini sasa jaa hilo limefurika hakuna mahala pengine paliobakia kuweza kutupa taka.

**SFX:** **Walking along the road ……tembea barabarani**

**Monica:** Kwa nini kuna taka nyingi sana?

**Bw.Gitanga:** Ndiyo, kuna sababu mbali mbali. Kwanza watu wengi zaidi wanaishi katika miji yetu. Tuchukulie mfano Manbarra ambao uko kilomita 20 tu kutoka hapa ambapo miaka 20 iliopita kulikuwa na watu 250,000 tu waliokuwa wakiishi kwenye mji huo na hivi sasa kuna takriban watu milioni moja hapo. Kila mtu huzalisha taka… na kadri tunavyozidi kutoa taka nyingi inabidi pia tuzitokomeze taka hizo.

**Moses:** Je hatuwezi kuziunguza taka hizo?

**Bw.Gitanga:** Bila ya shaka tunaweza. Utaratibu huo unaitwa uchomaji taka wa hadi zinapogeuka majivu.

**Moses:** (*excitedly ……kwa msisimko* ) Kwa hiyo hilo ndio jibu?

**Bw. Gitanga:** Sio lazima kusema huo ndio ufumbuzi. Wakati unapounguza taka za aina nyingi kama vile za plastiki huwa unatoa moshi wa sumu ambao huchafua mazingira, jambo ambalo ni baya kwa afya zetu. Pia utaratibu huo ni wa gharama zaidi kuliko hata wa kutupa taka kwenye majaa. Lakini hasa kile tunachotakiwa kufanya ni kutumia upya zaidi taka zetu.

**SFX:** **Coke can thrown into road …. kopo la Coke larushwa barabarani**

**Bw. Giatanga:** Liokote kopo hilo ambalo muuza duka amelirusha barabarani hivi punde. Huenda likawa limetengenezwa kwa jaribosi la aluminium. Naam tuendelee… unajua kwanza serikali inatakiwa ivilipe viwanda vyenye kuweza kutumia upya bidhaa mbali mbali ambazo tayari zimekwishatumiwa.

**Gladys:** Je kuna jambo lolote lile tunaloweza kufanya kuleta mabadiliko?

**Bw.Gitanga:** Bila ya shaka kutumia upya takataka kwa kuanzia majumbani. Unaweza kutumia upya vitu vya mboga mboga na mabaki ya chakula kutengenezea mbolea. Hiyo moja kwa moja itakuwa inamaanisha kwamba utakuwa unatupa taka chache. Pia unatakiwa utumie upya mifuko ya plastki na sio tu kuitupa ovyo.

**SFX: ( Hum of agreement …….mguno wa makubaliano)**

**Gladys:** Lakini nataka niwaonyeshe aina nyingine ya taka na kwa nini ni hatari.

**SFX: (throwing stones into water…..kurusha mawe majini )**

**Gladys:** Tazameni rangi ya maji! Kaka yangu anasema alikuwa amezoea pia kuvua hapa. Lakini anasema hivi sasa hakuna samaki yoyote aliebakia ndani ya mto huo.

**Moses:** Kwa nini hakuna ?

**Gladys:** Unaona viwanda vilivyoko pale… vile vyenye kutoa moshi mweusi… huwa vinachukua maji kutoka mtoni na wakati vinaporudisha maji hayo mtoni baada ya kuyatumia maji hayo tayari yanakuwa yamechafuliwa na kemikali.

**Moses**: (*incrediously ………kwa kutosadiki* ) Kwa hiyo unataka kusema kwamba yanaua mazingira?

**Bw. Gitanga:** Ndiyo yanauwa!

**Monica:** Sasa nimefahamu kwa nini uchafuzi wa mazingira ni jambo linalohitaji kuzingatiwa… kwa sababu sote tunayategemea mazingira.

**Moses:** Na iwapo tutaharibu mazingira tutakuwa tunapunguza kiwango bora cha maisha yetu wenyewe.

**Bw.Gitanga:** Ndiyo ni kweli.

**Music - 0:30**

**Je ulikuwa ukijua?**

Je ulikuwa ukijuwa kwamba katika ngazi ya dunia tunazalisha na kutumia zaidi ya tani milioni 100 za plastiki kila mwaka - hiyo ikiwa ni sawa na mifuko ya plastiki Billioni 120. Kwa kweli idadi hiyo ni mara 20 zaidi kuliko ile tuliotumia miaka hamsini iliopita. Sote huwa tunatumia mifuko hiyo aidha iwe mifuko ya plastiki ya maduka makuu ya bidhaa au chupa za maji za plastiki. Kwa miongo kadhaa mojawapo ya vivutio vikuu vya plastiki ni

kwamba bei zake ni za chini kwa kulinganishwa na vitu vingine. Lakini utokomezaji wa taka zake umezidi kugharimu mazingira. Plastiki nyingi huwa hazivundiki na bakteria. Kwa maneno mengine viumbe hai hawawezi kuzifanya zioze. Lakini watu wangapi kati yetu wanafikiria juu ya kile kinachotokea kwa bidhaa zetu za plastiki mara baada ya kuzitupa. Mifuko ya plastiki inatupwa ovyo na kuwa taka kwenye viunga vya Afrika na kwenye maji ya ufukweni na kama matokeo inauwa wanyama pori.
Kila mwaka zaidi ya viumbe bahari 100,000 kama vile nyangumi na pomboo wanakufa baada ya kudhania kwa makosa mifuko hiyo kuwa chakula. Hapo mwezi wa April mwaka 2002 nyangumi aliyekufa alipatikana kwenye mwambao wa Ufaransa. Uchunguzi uligundua kwamba tumbo lake lilikuwa na zaidi ya kilo 800 za mifuko ya plastiki na vifurushi. Inaaminika kwamba iwapo utatupa mfuko wa plastiki baharini utaelea kwenye bahari za dunia kwa zaidi ya miaka

mia nne na hamsini. Lakini hakuna mtu anayejua kwa uhakika juu ya hilo kwani plastiki hazikuwepo kwa muda mrefu sana duniani. Jambo la uhakika ni kwamba bidhaa zaidi na zaidi za plastiki hususan vifurushi vya plastiki kwa haraka vinajaza majaa yetu ya taka. Makundi ya kampeni yanasisitiza kwamba kuna mbadala wa kutumia mifuko ya plastiki. Idadi ya nchi zinazozidi kuongezeka zimekuwa zikitunga sheria kupunguza matumizi ya mifuko ya plastiki. Rwanda ni mojawapo ya nchi kusini mwa jangwa la Sahara barani Afrika kupiga marufuku mifuko ya plastiki. Nchi nyingine duniani zinapanga kuanza kutoza kodi kwa matumizi ya mifuko ya plastiki.

**Outro …….Funga kipindi.**

Na hapo ndio tumefikia  mwisho wa kipindi chetu cha Sikiliza na Ujifunze juu ya mazingira ambapo leo tumelenga takataka. Kumbuka kwamba unaweza kuleta mabadiliko nyumbani kwa kule tu kutumia upya mifuko na chupa za plastiki na kwa kuzigeuza mbolea taka zako za mboga mboga.

Ahsante kwa kuwa nasi.Iwapo ungelipenda kusikiliza tena kipindi hiki au kuwaelezea marafiki zako tafadhali nenda kwenye tovuti yetu www.dw-world.de/be
Kwaheri.